# KUWA KATIKA UPENDO NA YESU

Warumi 5:5, "…………. *Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi"*

Ule upendo wa Mungu unalia kama kengele ndani ya moyo wako, na unajua kwamba umepita kutoka mautini kuingia uzimani, unampenda kila mtu, na dunia yote imekuwa tofauti kwako, nawe umetia nanga pale, hakuna kitu cha kukusogeza wewe. Kuwa tu na furaha na uendelee mbele. Utukufu kwa Mungu. Usiache kitu kikusogeze/ kikugeuze hapo. Oh, unaweza ukatoka nje, na kuwa baridi, na kutingishwa kwa kiasi kidogo, lakini ile mbegu ya Mungu itabakia aminifu
(1 Yohana 3:9 – 10). Biblia ilisema, "Kama sisi hatuamini, Hata hivyo yeye, hataweza, Ni mkweli, atasimama kwa uaminifu" (2Tim. 2:11 – 13) [1]

Sikiliza, kwanza inabidi uzaliwe mara ya pili kwa Roho wa Mungu (Yohana 3:3). Kama sivyo hutaweza kuelewa Neno la Mungu. Mungu amesema hivyo. Mungu amesema, "Nimeificha Biblia kwa wenye hekima na akili na ninaifunua kwa watoto wachanga wawezao kuamini (Matayo 11:25). Kama unataka kupata kitu chochote kutoka kwa Mungu, kuwa kama mtoto. Fungua Biblia kuwa katika upendo na Yesu.

Biblia, inabidi usome katikati ya mistari, kwa sababu Mungu amewaficha wale wasomao Neno peke yake. Ninakariri maandiko kwamba amewaficha wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto ambao watajifunza (1Kor. 3:1 – 2). Wote waliosoma hilo katika Biblia waseme "Amina". Hivyo ni watoto wawezao kujinyenyekesha wenyewe, siyo wanaojiinua, lakini wawezao kujinyenyekesha na kusema, "Bwana ninaamini hilo". [2 ]

Huo ndio ushahidi kuwa, umepita kutoka mautini, Kuingia uzimani, Ndugu, (Yohana 5:24). Na vitu vyote vile ulivyowahi

kuvifanya, vimepita kabisa, kwa sababu uhai wa Yesu Kristo umemweka Roho Mtakatifu ndani, kukutawala wewe kiumbe kipya (2Kor 5:17). Na baada umesafishwa huna shauku tena ya dhambi muda wote uishio hapa duniani (Waebrania 10:2).

Sasa kama wewe ni mdhaifu wa kudumu na kuanguka na kuinuka juu kumbuka, umekuwa pengine na kule kulipokea kwa akili, lakini kamwe hujapata ule uzoefu/ ushuhuda wa kuzaliwa mara ya pili, ambapo upole, utu wema, na subira vinachukua mahali pa theolojia ya ki akili. Oh, unasema, "Sikiliza hapa, Ndugu

Branham, Ninajifunza Biblia. Mchungaji na kadhalika, nimechukua masomo ya Biblia".



Ndiyo, hata shetani naye pia, anajua mengi juu ya hayo utakayoweza kujua. Hiyo ni kweli. Lakini kuna jambo moja. Hawezi akapokea Roho Mtakatifu. Wewe unaweza. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo ili mradi hawezi kukupata…… kwa maana umekufa, maisha yako yamefichwa ndani ya Mungu. Na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu (Kolosai 3:1-4). Atawezaje kukupata wewe? Kitu cha kwanza, umekufa. Je umemsikia mtu aliyekufa akisema uongo? Umewahi kumsikia mtu aliyekufa akizoza na wewe? Simama katika kaburi uzoze naye usiku kucha, hatasema neno – kamwe. Kwa nini? Amekufa (Wagalatia 2:19-20) .
Na unajihesabu mwenyewe umekufa (Rumi 6:5-11), na maisha yako yamefichwa ndani ya Mungu kupitia Kristo , na kutiwa mhuri na Roho Mtakatifu. Njia pekee Shetani awezayo kukupata, itampasa apitie hatua zile zile za kuoshwa ambazo umezipita, na akapokee Roho yule yule uliyempokea, na sasa atakuwa ni ndugu yako Unaona?.

Kwa hiyo hawezi kukupata. Ni wewe ambaye hujaja kwa Yesu Kristo kwa kuanzia. Umefika mahali, sema, " Vema, unajua ndugu Branham, Bwana hajanitakasa mimi kutoka jambo hili".

Kama amekutakasa wewe na jambo moja, amekutakasa na mambo yote (Waebrania 10:10, 14;13:12). Anachukua nafsi yako yote, mwili, na roho (1Wathesalonike 5:23-24). Hiyo ni kweli. Usidanganyike ndugu. Kwa hiyo kama wewe unadumu katika kupanda juu na chini, kumbuka ndugu, bado hujaja kwa Yesu Kristo kwa usahihi bado.

Biblia ilisema, " msiipende dunia, wala mambo ya dunia". Na kama mnaipenda dunia, upendo wa Mungu hata haumo ndani yenu (1Yohana 2:15-17) umesisimka tu, na uamsho wa kiakili kwa mambo ya kikanisa, aina Fulani ya theolojia ambayo umefundishwa, na kamwe katika maisha yako hujakutana uso kwa uso , na Yesu Kristo, na kuzaliwa mara ya pili. Kwa maana ukiwa kwenye upendo wa Kristo, Dunia inakufa hapo hapo na milele.

Kwa maana umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu mpaka siku ya Ukombozi, na umekufa, na uhai wako umefichwa ndani ya Mungu kwa Kristo, na kutiwa muhuri pale na Roho Mtakatifu (Waefeso 4:30) unako kwenda kumejulikana hapo hapo, unapotiwa muhuri na Roho Mtakatifu [3].

Mara nyingine tunachanganyikiwa juu ya uzuri ni nini. Tunachanganyikiwa juu ya huruma ni nini, **huruma ya upendo**. Angalia hili kwa muda juu ya **huruma** wangapi wanaamini kwamba Yesu Kristo alikuwa na huruma? Kwa nini, hakika yeye alikuwa.

Sasa, Yeye alienda chini kwenye kisima cha Bethisida, na pale walilala jamii kubwa ya watu. Inachukua watu elfu mbili kufanya jamii moja. Na hapa palikuwa na jamii kubwa ya watu wamelala pale, viwete, vipofu, vilema, waliokaukiwa, wanangojea maji yatibuliwe. Na Yesu akaangalia jamii ile kubwa ya watu mpaka akamwona mtu ambaye, vema, hakuwa kiwete akasema, "Ninapoenda kule chini kwenye kisima, mtu mwingine huingia mbele yangu" (Yohana 5:1-15).

Ugonjwa wake, alikuwa nao kwa miaka thelathini na nane; haukuwa unaenda kumuuwa. Umedumaa, pengine TB, au shida ya kokwa, au kinginecho, na alilala chini. Na Yesu akamponya, naye akaenda zake na kuacha lile kundi kubwa la watu waliokuwa ukiwa, vilema, na viwete na vipofu (hiyo ni kweli?) na bado alikuwa mwingi wa huruma, mkombozi mwenye huruma. Uliona kile alichosema walipomuuliza juu ya hilo katika mstari wa 19 alisema, "Amini, Amini, nawaambia, mwana hawezi kutenda mwenyewe ila lile analomwona Baba analitenda" (Yohana 5:19-20).

Huruma ni kufanya mapenzi ya Mungu. Na hiyo hasa ndiyo huruma ya Kristo ilivyo, ni kufanya mapenzi ya Mungu. Tunaichanganya leo. Tunaweka ile hali ya kibinadamu pale.

Kama katika upendo, tunajaribu , kutumia upendo, upendo wa Mungu, kama upendo wa kibinadamu. Huwezi kuwa katika upendo na Mungu kama ufanyavyo kwa mkeo. Huwezi kuwa katika upendo na Mungu kama ufanyavyo kwa mume wako au msichana wako, au mvulana wako. Ni upendo wa aina mbili tofauti. Hata katika maneno ya kigiriki uko tofauti. Mmoja wao huitwa fileo; ambao ni upendo ulio na wivu….. lakini upendo wa Agapao, ambao ni upendo wa kiungu: baadala ya kuuwa mtu, itakufanya uombe kwa ajili ya nafsi yake yenye dhambi. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo jinsi unavyotofautiana.

Na tunafanya ile ya kibinadamu ichanganywe na ile ya Kristo, ile ya Kimungu, na tunapata mchafuko kutokana na hiyo. Kwa sababu, tunafahamu kwa inchi, futi, maili na kadhalika, kwa onzi, na paundi na kadhalika; hivyo ndivyo tujuavyo. Sisi ni watu wa wakati. Mungu ni wa milele; Yeye hana Inchi, hana maili, hana jana, au kesho. Yeye kwake ni milele. Na tunajaribu kuleta akili za milele za Mungu na kuzilinganisha na akili zetu zenye kikomo. Na, oh, tunachanganyikiwa. Kwa hiyo njia nzuri ya kufanya, ni kusoma Neno lake; na kukumbuka kwamba Neno lake halipingani [4 ].

Sasa unajua kile alichofanya? Kama utaangalia …….. sasa, ninajua wengi wanaweza wasikubaliane nalo. Kama ni sawa tu kuzungumza hili, unaona mimi…… itakuwa tu ni mawazo yangu Mwenyewe. Unaona, Biblia ni kitabu cha kimiujiza kimeandikwa kwa namna ambayo Kimefichwa kwa mashule, watheolojia. Ni wangapi wanajua hilo? Yesu alimshukuru Mungu. Alisema, "nakushukuru Baba kwakuwa mambo haya umewaficha wenye hekima na akili ukawafunulia watoto wachanga walio tayari kujifunza".
Ni kitabu cha upendo. Wakati upendo wa Mungu unapoingia moyoni, unakuwa katika upendo na Mungu. Ndipo anajifunua mwenyewe. Biblia, maana ya tafsiri ya biblia ni Mungu mwenyewe akitafsiri ahadi yake. Lakini Biblia imeandikwa katikati ya mistari.

Sasa, kama mke wangu, oh ni mwanamke wa ajabu sana katika dunia nzima, na ninampenda sana. Naye ananipenda. Sasa ninapokuwa mbali na nyumbani, ataniandikia barua, na kusema, "Mpendwa Billi, usiku huu nimemaliza tu kuwafanya watoto walale. Nimefua leo," na mambo yote aliyofanya nakadhalika. Sasa, anasema hayo katika barua. Lakini unaona, ninampenda yeye sana, natumekuwa kama mtu mmoja, mpaka ninaweza kusoma katikati ya mistari. Ninajua anachotaka kusema, hata kama amesema au hakusema. Unaona, ninajua anachomaanisha, kwa sababu ni upendo wangu kwake, nami ninaelewa.



Vema , hivyo ndivyo Biblia ilivyoandikwa unaona? Waliosoma litawapita juu hilo. Hawawezi kamwe kulipata. Unaona? Inabidi uwe katika upendo na Neno, ili kumjua Yeye (Yohana17:3) [5]

Sasa, ninakubali kuwa watu, wanajifunza sana, na wanajaribu kwenda mbali mbele, na kufikiri kwa bidii sana, na mara nyingine wanarukwa na akili na mambo kama hayo, kwa kujifunza juu ya Bwana. Lazima uachane na hilo. Hupaswi kufanya hivyo. Jambo pekee upaswalo kufanya ni kuwa katika mapenzi na Yeye. Na kuendelea kumpenda Yeye. Amina.

Sio kujaribu kujisukumiza kwenye jambo Fulani au kujifanya kitu Fulani ambacho sicho ulicho" wewe endelea tu mbele na umuache Mungu akutumie kwa namna anayopenda yeye. Jisalimishe mwenyewe; jikabidhi mwenyewe na utembee tu, mwenye furaha, unaimba na kushangilia (Mithali 8:17) [6].

Hivyo ndivyo ilivyo na Mungu. Hatujaribu kujifunza kutoka katika gazeti lenye msimamo Fulani, mtazamo, Fulani , wa Kitheolojia. Lakini kuwa katika upendo naye. Nenda magotini na umpate Yeye moyoni mwako.

Upendo wa Mungu umemiminwa moyoni mwako na Roho Mtakatifu (warumi 5:3-5) Halafu unaenda kusomo Biblia. Unaiona inakuja hasa katikati ya mistari. Unaona, kile anachosema. Hajasema hicho wazi katika Neno.

Sasa, hakuna mtu mwingine awezaye kusoma barua ya mke wangu kama hivyo, kwa sababu nampenda hivyo. Unaona? Na ndivyo Yeye anavyo niandikia mimi. Hivyo ndivyo anavyokuandikia wewe; ni katikati ya mistari. Nawe unasoma hayo. [7]

Lakini kama unasoma katikati ya mistari na kujaribu kuifanya iseme jambo Fulani, ambalo liko katikati ya mistari na linasema tofauti na yale ambayo mistari inasema, hapo uko makosani. Lakini ni lazima ikubaliane, kwa kupitia yote yaliyo andikwa [8].

Kama unataka kuwa mtu wa maana katika kanisa lako, kanisa lolote unalokwenda, wewe kuwa katika upendo na Mungu kwa moyo wako wote (Matayo 22:34-40) na unapofanya hivyo, utakuwa katika upendo na kila mtu wa kanisa lako na kila mtu wa Kanisa lolote lingine kwa moyo wako wote.

Sasa huwezi ukadanganya kwa hilo. Sasa kuna kitu fulani juu ya hilo ambacho watu wanakifahamu. Kama kunajambo lolote ambalo naweza kuchangia juu ya mafanikio

ya mikutano yangu, tukizungumza kama wanadamu, nikujua kwamba watu wanafahamu kwamba ninawapenda watu kweli. Na hilo wanalijua. Huwezi kuwadanganya watu juu ya hilo. Kama unaigiza hilo au unajifanya.

Kama vile tu Ukristo, kama unaigiza umkristo – au unajifanya hasa, kuwa ni Mkristo, hutaweza kuendelea kamwe na huo. Hapana Bwana. Ni lazima kiwe ni kitu halisi pale. Hilo tu. Upendo utalifanya hilo (1Tim. 1:3-5) [9].

Nabii wa Mungu alizungumzia habari za mtu ambaye mkewe alikuwa karibu afe na saratani (kansa), alijua Mungu anaweza kumponya. Kama Mungu angelimponya mkewe angemponya na mvulana, ilifanya waingie katika hali ya kutaharuki. Unaona? Lazima uje, na unapokuwa katika hali ya kutaharuki hapo sasa Mungu atakusikiliza wewe. Lakini kama ni mlegevu, hujali kama atafanya au hatafanya, vema sasa, hiyo ni tofauti. Unasema unajali, lakini inahitaji kung'ang'ania ili alifanye hilo.

Sababu inayoacha hakuna kung'ang'ania ninaamini ni kwa sababu ya kukosa upendo, upendo wa Mungu. Nafikiri kwamba upendo wa Mungu husababisha kung'ang'ania. Kama Mungu yuko ndani yako, ile ishara ndani yako, na unaona hali za wakati na watu wanavyoishi kwenye dhambi jinsi walivyo, itakuingiza katika hali ya kung'ang'ania. Naamini itafanya hivyo.

Sasa Neno kwa uwazi linasema hivi katika Wagalatia 5:6, Imani itendayo kazi kwa upendo. Na njia pekee iwezayo kukufanya uwe na Imani, ni kuwa na upendo kwanza. Kwa sababu hata hivyo imani ni motisha ya upendo. Motisha, hivyo ndivyo hasa Imani ilivyo, ni motisha kwa upendo. Sasa, kama huna upendo huwezi ukawa na Imani.

Wawezaje kuwa na Imani kwa mke wako kama humpendi? Huo ni upendo wa fileo. Sasa, ni vipi upendo wa Agape (Agapao) kwa Mungu? Utawezekanaje kama humpendi Mungu? Kama unasema unampenda mke wako nawe hujamwambia hilo kamwe, na kamwe hujakaa naye chini na kufanya mapenzi naye, kulieleleza kwake, kumbusu, kumkumbatia, na kumwambia yeye ni mpishi mzuri katika nchi yote, mambo yote unayoyajua, na jinsi alivyo mzuri, na kwa kiasi gani unampenda; kama hufanyi hivyo hatajua hilo kamwe, hiyo ndiyo njia. Kama unampenda yeye unalieleleza.

Hivyo ndiyo tufanyavyo kwa Mungu. Tunapompenda Yeye, tunamueleza Yeye juu ya hilo. Tunakaa chini na kumwabudu Yeye, na kumsujudia Yeye. Na……. Unaona, upendo unatuendesha kufanya hilo (2 Korintho 5:14) [ 10 ].

"Efeso" maana yake, jina lenyewe, Efeso maana yake iliyoachilia, legea, rudi nyuma." Liliitwa na Mungu," Kanisa lililorudi Nyuma. Mungu alisifu kwanza matendo yake ya kwanza, kazi zake, na subira yao. Mungu ana wakemea kwa kuacha upendo wao wa kwanza, kwa kurudi nyuma na kuacha kuangaza. Efeso sio kanisa lililodanganywa; lilishindwa lenyewe kwa kutoendelea na upendo mkamilifu ufunuo 2:2-6.

"Lakini nina Neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza," Ili kufahamu jambo hili huna budi kutambua ya kwamba Roho haneni na wale watakatifu wa kwanza wa Efeso peke yao. Ujumbe huu ni kwa ajili ya wakati wote mzima uliodumu kwa muda wa kama miaka 120. Ujumbe wake, basi, ni kwa ajili ya vizazi vyote katika kipindi hicho. Sasa historia inafululiza kujirudia yenyewe. Katika vizazi vya Israeli tunaona mioto ikififia katika kizazi kinachofuata. Katika kizazi cha tatu, makaa ya moto huenda yanamweka kidogo, lakini katika cha nne huenda kusiwe na dalili ya mabaki hata kidogo ya ule mwali wa mwanzoni. Basi Mungu anauwasha moto tena, halafu tendo lile lile linarudiwa. Kwa urahisi tu ni dhihirisho la kweli ya kwamba Mungu hana wajukuu. Wakovu haupokezanwi kwa kuzaliwa kimaumbile kama kusivyo na ukweli hata kidogo wa uhalifa wa kimitume. Haliko katika Neno. Unaanza na waamini waliozaliwa kweli mara ya pili, na wakati kizazi kinachofuata kinapokuja wao ni Wabatisti, Wamethodisti, n.k. hivyo ndivyo hasa walivyo, pia. Wao si Wakristo. Huna budi kuzaliwa kwa mapenzi ya Mungu. Sisemi ya kwamba wengine wao hawako sawa na Mungu. Sisemi hivyo hata kidogo, lakini ule moto wa kwanza umezima. Wao hawako vile walivyokuwa tena.

Ile shauku kali ya kumpendeza Mungu, shauku ya kutaka kulijua Neno lake, kilio cha kumtafuta Roho, yote yanaanza kufifia na badala ya kanisa hilo kuwaka kwa moto wa Mungu, limepoa na kuwa la kawaida kidogo. Hilo ndilo lililokuwa likitukia kule nyuma kwa Waefeso. Walikuwa wanakuwa wa kawaida kidogo. Kule kujulikana kwao kwa ajili ya Mungu kulikuwa kunafifia na watu hawakujali sana yale Mungu aliyowawazia kwa kuwa walianza kujali yale ulimwengu ulichowawazia. Kizazi cha pili kilichofuata kilikuwa tu kama Israeli. Walitaka wawe na mfalme kama mataifa mengine. Walipofanya jambo hilo, walimkataa Mungu. Lakini walifanya jambo hilo hata hivyo. Hiyo ndiyo historia ya kanisa. Wakati linapowazia zaidi juu ya kufanana na ulimwengu badala ya kufanana na Mungu, haichukui muda mrefu kabla hujawaona wakiacha kufanya mambo ambayo wao wasingeyafanya hapo awali.

Wanabadilisha namna yao ya kuvaa, njia zao na mienendo yao. Wanalegea. Hiyo ndiyo maana ya "Efeso:' kulegea – kuelea.

Mzunguko huo wa ufufuo na mauti haujafa kamwe. Unalohitaji kufanya tu ni kukumbuka tukio hili lililopita la Mungu katika Roho, wakati wanaume na wanawake walipovalia kama Wakristo, walienda kanisani, wakaomba usiku kucha, wakaenda pembeni mwa barabara nao hawakuonea haya kuhusu madhihirisho ya Roho. Waliyaacha makanisa yao ya kale yaliyokufa na kuabudu nyumbani ama kwenye majengo ya maghala ya kale. Walikuwa na kitu halisi. Lakini haikuchukua muda mrefu sana hata walipoanza kupata pesa za kutosha kujenga makanisa mazuri mapya. Waliweka kwaya badala ya wao wenyewe kumwimbia Mungu. Waliwavalisha wana kwaya majoho. Waliunda Mashirika na kusoma vitabu visivyostahili kusomwa. Waliacha milango wazi na mbuzi wakaingia na kutawala. Zile kilele za furaha zilikuwa zimekwisha. Uhuru wa Roho ulikuwa umeondoka Loo!

Waliendelea na desturi; lakini ule moto ulikuwa umezimika na weusi wa majivu ndio karibu tu uliobakia.

Muda kidogo uliopita nilisema ya kwamba Yohana alifahamu kumpenda Mungu ni kitu gani. Huyo mtume mashuhuri wa upendo bila shaka angeona jambo hilo wakati kanisa lilipoanza kupoteza upendo huo wa kwanza wa Mungu. Katika (1Yohana 5:3), yeye anasema, "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake (Neno lake)," Kuchepuka kidogo kutoka kwenye Neno hili kulikuwa ni hatua moja kutoka kwa Kristo. Watu wanasema wanampenda Mungu., wanaenda Kanisani, hata wanapiga makelele na kufurahi na kuimba nakuwa na wakati wa furaha na kuchemka. Lakini hayo yote yanapokwisha, wewe angalia uone kama wako kwenye hilo NENO, wakienenda katika hilo, wakiishi ndani yake. Kama wakipitia katika hayo mengine yote na kisha wasiende katika Neno hilo, wanaweza kusema wanampenda Mungu bali maisha yao yanasimulia hadithi nyingine. Sijui kama Yohana hakuona mengi ya hayo kabla hajafa; watu wakisema walimpenda Mungu lakini hawatii Neno lake. Loo! Kanisa la Efeso, jambo Fulani limewapata. Mtu Fulani anajaribu aidha kuongeza kwenye Neno hilo ama kuondoa kwake. Lakini wao wanafanya tendo kubwa sana hata huwezi kuliona huko nje waziwazi. Limejificha na wanalileta kwa njia ya hoja na ufahamu wa kibinadamu na litashinda, labda mlikatae. Rudini Pentekoste kabla ya kuchelewa!.

Lakini kama kawaida watu hawasikii onyo la Mungu. Huo moto wa ufufuo uliowashwa juu ya Neno takatifu ni mzuri sana, na dhihirisho la Roho limebarikiwa sana, hivi kwamba uongo mdogo unapenya ndani unapenya ndani na mnog'ono moyoni unasema, "Tunawezaje kuilinda kweli tuliyo nayo?" Hapo ndipo roho ya "mpinga – Kristo" inapoingia na kunong'oneza, "Angalia, mnayo ile kweli sasa, angalieni isipotee. Undeni madhehebu na mworodheshe kanuni zenu za imani mnazoamini. Ziandikeni zote katika kitabu kidogo cha mafundisho ya Kanisa." Nao wanafanya hivyo. Wanaunda madhehebu. Wanaongeza kwenye Neno. Nao wanakufa kama tu Hawa alivyofanya kwa

kuchukua Neno moja lisilo sahihi. Neno la Mungu ndilo linaloleta uzima. Na si kutumainia yale tusemayo kuhusu Neno , bali ni yale aliyosema Mungu. [11]

Imekuwa ni jambo kubwa kwangu Tangu litokee kwangu .
(Wakati Nabii wa Mungu alipokuwa nyuma ya pazia la wakati).
Sijui, ninapofikiria pale, niliposimama pale, kwa wakati ule wa furaha kuu, nami nikafikiri "Hakuna kesho". Hakukuwa na Jana; hakukuwa na ugonjwa, hakukuwa na huzuni. Hakukuwa na furaha kidogo, na halafu furaha kuu, yote ilikuwa ni furaha nyingi sana, yote ni furaha Oh jamani, niliposimama pale, na nikasema, hii ni nini? (1Kor 2:9-10).

Ile sauti ilisema, "Huu ni upendo mkamilifu, na kila kitu ulichowahi kukipenda na kila kitu kilichokupenda wewe kipo hapa pamoja nawe sasa".

Hii asema Bwana, itachukua upendo mkamilifu ili kukuchukua wewe mahali pale, kwa maana huo ndio uliokuwapo pale, haijalishi ni wangapi, kiasi gani cha madhihirisho ya kidini, ni vitu

vingi vizuri vingapi ulivyovifanya au chochote ulichofanya, hilo halitahesabika. Katika siku hiyo . Itachukua Upendo wa Mungu mpaka uweze kuwapenda wale wanaokuchukia wewe (Matayo 5:43-48) [12].

Lakini simtumikii Bwana kwa sababu nafikiri atanipeleka mimi kuzimu nisipo mtumikia; ninamtumikia kwa sababu ninampenda Yeye. Ninamtumikia kwa sababu kuna kitu Fulani ndani yangu. Kama unatoka nje na kusema," vema inabidi niache kufanya hivi kwa sababu kanisa langu haliamini hilo" unachukua tu nafasi ya mnafiki. Hiyo ni kweli. Lakini kama unalifanya hilo kwa sababu unalipenda hilo, na ni mchango wako kwa Mungu, na kitu Fulani ndani ya moyo wako kilifanya, upendo wa Mungu kwako uwe mkubwa kuliko mambo haya mengine, sasa hapo uko kwenye mstari sahihi. Lakini kama silewi, sivuti, kutafuna, kulaani, wala chochote kile, bado nitaenda kuzimu hakika. Nimejiunga na makanisa yote, nimebatizwa, na jina langu liko katika kila kitabu na nikawa na nafasi ya muhimu, na nikaishi maisha mazuri, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kamwe kuuona ufalme wa Mungu (Yohana 3:3) Hiyo ni kweli. [13 ].

Sasa Mungu anamjua kila mmoja wetu, hivyo kama atakuja usiku huu wa leo na akauleta mara ya pili uhai wa Mwanae Yesu Kristo katika kanisa, hapo utampenda zaidi na zaidi na zaidi wakati wote. Kuwa katika upendo na Yeye na umweke Yeye moyoni mwako. Na usiangalie watu wanasema nini. Wewe endelea tu katika upendo na Kristo Yesu, naye atakuongoza kwenye majani mengi yalio mazuri. Mungu akubariki wewe [14 ].

**Nukuu za kiingereza**

*[1] Israel wakiwa Misri Aya 136*
*[2] Ibrahimu (55 – 0624, Zurich). Aya 22 – 23*
*[3] Torati ikiwa ni kivuli Aya 57 – 59*
*[4] Msikieni Yeye (60 –0712), Klamath falls ) Aya 5 - 7*
*[5] Kumiliki malango ya Adui 64-0322. Denham sp) Ays 9 –10*
*[6] Maswali na majibu (54-0103m), Aya 140*
*[7] Jehovayire sehemu ya 3"(64-0404, Louisville) Aya 44.*
*[8] Jehova yire (59-0417), Aya 23 [9] Unaamini sasa (55-0610, macon), Aya 28-29*
*[10] Kung'ang'ania Aya 66-69 [11] Wakati wa kanisa wa Efeso ROJC Aya 73 + NSK U. 88-89*
*[12] Kufanywa wana (60-0522E), Aya 89 –90, Aya 89,104*
*[ 13] Maswali na majibu (59-0628E) Aya 114*
*[14] Mstari wa uponyaji (53-0907E, Chicago), Aya 4*

Jiwe la kiroho la kujengea no 145 kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa hii yamekusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69D, 75328 Schomberge, Germany simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724).

Kwa nakala zaidi andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe -  Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*